JARIDA MAALUMU LA MTANDAONI TOLEO LA PILI www.owm.go.tz FEBRUARI 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.





# Waziri Lukuvi amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Shirika la FAO



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa William Lukuvi amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) katika ukumbi wa Ofisi ya Waziri Mkuu uliyopo katika Mtaa wa posta Jijini Dodoma.

Ujumbe huo kutoka FAO umefanya ziara ya wadau wa ufadhili wa Mfuko Nyumbulifu wa Uchangiaji kwa Hiari (Flexible Voluntary Contribution - FVC) iliyohusisha Waheshimiwa Mabalozi wa Ubelgiji na Uswisi, Wawakilishi wa Kudumu FAO katika Umoja wa Mataifa, Rome, Washauri Waandamizi wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDC) na Viongozi Waandaamizi wa FAO Makao Makuu.

Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuwezesha washirika (partners) kupata uelewa wa utekelezaji wa programu na miradi inayofadhiliwa kupitia Flexible Voluntary Contribution (FVC) nchini Tanzania, kuongeza uelewa, muonekano na fursa zinazopatikana kwenye FVC kama mfuko nyumbulifu wa utoaji misaada ili kuweza kufikia malengo ya kimkakati Kitaifa na Kimataifa kupitia FAO.





# Taarifa za awali za taadhari za maafa zitoke kwa wakati



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. William Lukuvi ameelekeza Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kujiratibu vizuri katika kufikisha taarifa zote za taadhari ya maafa kwa wakati ili utekelezaji wake ufanyike mapema kabla ya madhara kutokea.

Kauli hiyo ametoa leo alipotembelea Kituo cha Ufuatiliaji wa Majanga Katika Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura Kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu, Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

" kwa nafasi mliyonayo na teknolojia mnazotumia mnaweza kujua na kutoa taarifa zote za tahadhari bila urasimu, ili kuepuka athari kubwa za maafa zinazoweza kutokea baadae."alisisitiza Waziri Lukuvi.

Aidha muangalie na uwezekano wa kurahisisha mawasialiano ya taarifa zote za tahadhari ziweze kupatikana kila siku kwa njia ya simu ili kila mtu anayeenda kwenye shughuli ajue na achukue tahadhari.

“huduma hii iwe bure na ipatikane muda wote ili wananchi waingie wasome na wachukue tahadhari, na tutakuwa tumefanya kazi yetu vyema,” alisema

Naye Mkurugenzi Msaizidizi anaye simamia Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Bi: Jane Kikunya amelezea kuhusu ufanyaji kazi wa kituo hicho kwamba kinajukumu kubwa la kufuatilia majanga ikiwa ni pamoja kushirikiana na taasisi mbalimbali katika ngazi ya kitaifa katika kutoa taarifa za awali za tahadhari kwa ngazi mbalimbali.

Amefafanua kwamba katika Ngazi ya Mikoa kuna vituo vya maafa vinapaswa kuanzishwa na jukumu hilo limeainishwa katika sheria ya maafa ya mwaka 2022 ambayo imeeleza kila Mkoa, kuwa na kituo cha usimamizi wa maafa ili kufanya ufuatiliaji wa majanga yanayoweza kutokea katika eneo la Mkoa husika.

Hivyo Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya ufuatiliaji wa uanzishwaji wa vituo hivyo ambapo wameweza kukutana na Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa ambao kisheria wamepewa jukumu la usimamizi wa vituo hivyo ili kujengeana uelewa wa miongozo na namna ya uanzishaji na usimamizi wa vituo hivyo.

.





Serikali Yazindua awamu ya tatu ya mradi wa timiza malengo kupambana na VVU




Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Nderiananga, kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amezindua awamu ya tatu ya mradi wa Timiza Malengo 2024-2026 unaotarajiwa kutekelezwa katika Mikoa 10 na Halmashauri 36 nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Mhe. Ummy amesema kuwa mradi wa Timiza Malengo unalenga kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) kwa vijana balehe wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 24 walio mashuleni na nje ya mfumo wa elimu kwa kuwajengea uwezo wa kujikinga dhidi ya maambukizi na kuwawezesha kiuchumi katika Mikoa ya Singida, Lindi, Morogoro, Njombe, Dodoma, Tabora, Tanga, Ruvuma, Geita na Mara.

Mhe. Ummy ameeleza kuwa serikali inaendelea na mipango ya kisera na kimuundo kuhakikisha hadi ufikapo 2030 Tanzania iwe imefanikiwa kufikia 03 katika mapambano dhidi ya maambukizi mapya, kuzuia vifo vitokanavyo na VVU/UKIMWI pamoja na unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na maambukizi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dkt. Catherine Joachim, ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutekeleza mradi huo, akibainisha kuwa itawafikia vijana balehe walio katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU na kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi nchini.

Pia, Dkt. Catherine ameeleza kuwa mradi utasaidia kufikia malengo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika mapambano dhidi ya UKIMWI ifikapo 2030, kuongeza wigo wa utekelezaji wa afua za kinga kwa vijana, kutunisha mfuko wa udhamini pamoja na kuboresha mifumo ya uratibu.

Aidha, mradi wa Timiza Malengo kwa awamu ya tatu umelenga kuwafikia na vijana balehe wa kiume na kuwapa mafunzo stadi, kuwaunganisha na taasisi za ufundi hususan VETA, pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha zinazotoa mikopo nafuu ikiwemo mikopo ya 10% inayoratibiwa na serikali kupitia wizara ya TAMISEMI.




HATARI
DANGER

# Dkt. Yonazi Awakumbusha watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kutekeleza majukumu kwa weledi



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amewakumbusha watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ushirikiano, upendo furaha na Amani ili kuyafikia malengo ya Ofisi hiyo.

Dkt. Yonazi ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na Watumishi Ofisi yake wakati wa mkutano wake na watumishi hao uliofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi iliyopo Njedengwa Jijini Dodoma.

Dkt. Yonazi amesema ipo haja ya kila mtumishi kujifanyia tathmini katika utendaji wakewa kazi huku akizingatia miongozo na kanuni za utumishi wa umma na kusema kuwa, kila mtumishi anawajibika katika kuhakikisha ofisi inapata matokeo iliyoyakusudia na kwa ufanisi.

"Ni wakati sahihi kila mmoja kuilinda furaha aliyonayo awapo mahali pa kazi isingefaa utoke nyumbani huna furaha na ufike eneo la kazi ukose furaha, ni vyema kuja eneo la kazi na uipete furaha mara mbili kwa kuzingatia mazingira yaliyorafiki katika kutekeleza majukumu," alisma Dkt. Yonazi

Aliongezea kuwa kila Mtumishi wa Umma awe na desturi ya kuheshimu nafasi ya mwingine bila kujali tofauti zinazoweza kuwepo miongoni mwa watumishi hao.

Ni vyema kila Mtu akajali mwingine na ikumbukwe hakuna mtu mwenye uwezo mdogo wa kufanya kazi, jambo la msingi ni kuhakikish ule uwezo uliopewana Mwenyezi Mungu na mafunzo mbalimbali unatumia vizuri na kuhakikisha unaleta matunda mazuri na kuleta maendeleo kwa mchi yetu," alisema Dkt Yonazi

Sambamba na hilo aliwaeleza watumishi hao kuwa kila mmoja ni kiongozi katika eneo lake la kazi hivyo abebe dhamana hiyo kwa weledi na ufanisi mkubwa.

".... kila mtumishi aliyepo hapa ndiye Katibu Mkuu kwenye eneo lake, kwa kubeba imani ya kwamba ni Katibu Mkuu anapaswa kuwa na nidhamu na bidii katika kazi ikiwa ni pamoja na kuwa mwaminifu," alisema.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. James Kilabuko katika neno lake la utangulizi amewaasa Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi na kuzingatia sheria za utumishi wa Umma huku akiwasihi kuimarisha umoja na mshikamano ili kuiletea Serikali maendeleo yake.





Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480